JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS-TAMISEMI

Namba za Simu

Mkuu wa Shule: 0742 770 656
Makamu Mkuu wa Shule: 0767 312 266
Matron: 0766 464 076

Shule ya Sekondari Nsimbo,

S.L.P.304,
MPANDA.

Kumb. Na. NDC/NSS/JI/A.L/02

15/05/2018.

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……

S.L.P. ……

……..

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI NSIMBO, HALMASHAURI YA NSIMBO, MKOA WA KATAVI MWAKA 2018.

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2018 Katika tahasusi ya …… Shule yetu ni ya bweni na ni ya wasichana, ipo katika Halmashauri ya (W) Nsimbo mkoa wa Katavi.

Tafadhali wahi kufika maana ukichelewa zaidi ya wiki tatu (3) nafasi itachukuliwa na mwanafunzi mwingine. Shule itafunguliwa muhula wa kwanza tarehe 02/07/2018. Hongera kwa kuchaguliwa katika Shule hii, nakutakia maandalizi mema na safari njema.

Karibu Nsimbo Sekondari. Karibu Katavi.

……

BEATRICE A. MWALUGAJA

MKUU WA SHULE

YAFUATAYO NI MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE HII AMBAYO NI MUHIMU KUZINGATIA:

A. USAFIRI

Kila mwanafunzi atajitegemea kwa usafiri. Kwa wanafunzi kutoka Tabora kuja Mpanda (Katavi) kuna usafiri wa treni (gari moshi) na Mabasi, usafiri wa gari moshi toka Tabora kuja Mpanda (Katavi) upo kila Jumatatu, Jumatano na Jumamosi na kufika Mpanda Jumanne, Alhamisi na Jumapili. Pia kuna usafiri wa mabasi kila siku.

Usafiri wa kutoka Mbeya hadi Mpanda (Katavi) ni wa mabasi, unapatikana kwa mabasi ya Mbeya Express, Katavi tours, Ndenjela Epress na Mugumo Express kila siku. Na usafiri toka Kigoma ni wa mabasi, unapatikana kwa basi la Adventure Connection na Saratoga Line kila siku.

Ukifika Mpanda: I. Kutoka stesheni ya gari moshi shule iko mashariki umbali wa km 12 ukipiti barabara ya Mpanda Tabora. II. Kutoka kituo cha mabasi (stand kuu) shule iko mashariki umbali wa km 12 ukipitia barabara ya Mpanda Tabora. NB: Ili kukusisitiza usafiri wa kutoka Mpanda kuja shuleni usafiri ni wa daladala na bodaboda na uwaambie wakuteremshe Mtakuja maarufu TANKI REFU. III. Ukitokea Tabora kwa njia ya barabara huna haja ya kufika Mpanda mjini ukishaingia Halmashauri ya wilaya ya Nsimbo waambie wakuteremshe **Tanki refu**.

B. VITU MUHIMU VYA KUJA NAVYO;

1. SARE ZA SHULE

a) Kila mwanafunzi aje na Tsh. 32,000/= kwa ajili ya kitambaa na mashono ya sketi mbili za darasani na sh. 16,000/= sketi ya kushindia.

NB: Si jukumu la shule kushona sare za wanafunzi, mwanafunzi husika ataelekezwa kwa mtu aliyeteuliwa na shule kwa kazi hiyo. Utaratibu huu umewekwa ili wanafunzi wawe na sare zinazofanana. Wanafunzi wote watashona sketi ndefu. Kama mzazi utaamua kumshonea mwenyewe na rangi au mshono ukawa tofauti na shule, basi mzazi utalazimika kumshonea sare nyingine.

b) Shati nyeupe mbili 2 za mikono mirefu zisiwe na urembo wa aina yoyote, uvaaji wa shati utaambatana na hijab nyeupe kwa wanafunzi wa kiislam.

c). Sweta ya shule rangi dark - blue ya kawaida Sh. 13,500/= .

d). Viatu vya ngozi nyeusi vyenye kisigino kifupi vya kufunga kamba jozi 2.

e). Soksi fupi nyeupe jozi mbili na nyeusi jozi mbili.

f). Raba kwa ajili ya michezo nyeusi/dark blue jozi 2.

g). Aje na shilingi 13,000/= kwa ajili ya T-shirt ya shule

h). Track suit jozi moja kwa ajili ya kuvaa usiku wakati wa maandalio ya usiku/michezo, rangi ya dark blue 30,000/=

i). Aje na T-shirt ya njano ambayo haina maandishi yeyote kwa ajili ya michezo.

j). Tai ya rangi ya Dark blue

Malipo haya yote yawekwe kwenye Akaunti ya shule, **61910022051 NSIMBO SEC SCHOOL FUND Benki ya **NMB****

NB: MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUJA NA MAVAZI YA AINA YEYOTE ZAIDI YA SARE ZILIZOTAJWA HAPO JUU

II. ADA NA MICHANGO MUHIMU YA SHULE

a) Ada ya shule ni elfu sabini (Sh. 70,000/=) inaruhusiwa kulipa nusu yaani elfu thelathini na tano (Sh. 35,000/=) kwa kila muhula. Mwanafunzi atakaye fika shuleni bila ada atarudishwa nyumbani.

b) Sh. 5,000/= kwa ajili ya tahadhari

c) Sh. 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha

d) Sh. 20,000/= kwa ajili ya taaluma

e) Sh. 30,000/= kwa ajili ya vibarua (walinzi, wapishi n.k)

f) Sh. 2,000/= kwa ajili ya nembo ya shule

g) Sh. 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani

h) Sh. 20,000/= kwa ajili ya Mtihani wa Utamilifu (Mock) Mkoa.

i) Aje n ash 10,000/= kwa ajili ya mahafali

j) Aje na pesa sh. 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza pesa hiyo haitarudishwa.

NB: Ni vema mwanafunzi aje na bima ya Afya ya Taifa kwa ajili ya matibabu.

Michango yote tajwa hapo juu kipengele II a – j inatakiwa kulipwa benki, mwanafunzi aje na bank pay in slip (stakabadhi ya malipo ya benki) hakuna pesa ya mwanafunzi itakayo pokelewa shuleni. Michango hiyo pamoja na ada ilipwe kwenye akaunti namba **61910022051** ya **NSIMBO SEC SCHOOL FUND** katika benki ya **NMB Tawi la Mpanda**.

Benki ya **NMB** ipo kila makao makuu ya Wilaya unaweza kulipa katika tawi lolote lile la NMB.

NB: NYUMA YA BENKI PAY IN SLIP UANDIKWE MCHANGANUO WA MALIPO HUSIKA HAKUNA MWANAFUNZI ATAKAYE POKELEWA BILA BENKI PAY IN SLIP (NAKALA YA STAKABADHI YA MALIPO YA BENKI)

III. MALAZI

a) Godoro la sponge 2.5 x6 Na lisiwe nene sana (hakuna magodoro ya kukodisha)

b) Shuka jozi mbili rangi ya Pinki.

c) Mto na foronya ya rangi ya Pinki.

d) Blanketi moja/Shuka moja nzito

e) Aje na chandarua nyeupe pembe nne.

f) Taulo

g) Doti ya khanga au kitenge.

h) Nguo za ndani za kutosha

j) Pedi

IV. VITENDEA KAZI

a) Ream ya karatasi (1 kwa mwaka)

b) Jembe moja lenye mpini na fyekeo

c) Fagio 1 (hard bloom na soft bloom)

d) Mathematical set, pencel, rula n.k .

e) Ndoo 2 za plastiki (Kuogea na kutunzia maji ya kunywa) lita 20 na lita 10.

f) Fagio ngumu aina ya chelewa (1)

g) Mwanafunzi wa sayansi (PCB) na (CBG) Aje na dissecting kit, scientific calculator, stop watch, tray, laboratory coat, kwa mwanafunzi wa PCM aje na laboratory coat, scientific calculator na stop watch na kwa mwanafunzi wa HGE na EGM waje na scientific calculator.

h) Madaftari makubwa (Quire three) yasiyo pungua kumi (10)

V. TAALUMA

Kwa sababu shule ina uhaba wa vitabu, ikiwezekana ni vizuri aje na vitabu vitakavyo msaidia kwa masomo husika

A. VITABU VYA KEMIA

1. BYS. Chand conceptual chemistry for class XI and XII

2. BY Tanzania institute of education ADVANCED LEVEL INORGANIC CHEMISTRY part I and II

3. Advanced chemistry review (2000) – (2012) Paper I & II

4. Advanced Chemistry (Michael Ramsden)

B. VITABU VYA BIOLOJIA

1. Taylor at el (1999) biological science, third edition. Tong printing press hong kong

2. Genn and Tods (1999) Understanding biology 4th Ed. Stanley Thomes Ltd UK.

3. MODERN BIOLOGY SECOND EDITION

4. FUNCTIONAL APPROACH

5. ADVANCED BIOLOGY BY MICHAEL KENT SECOND EDITION

C. VITABU VYA PHYSICS:

1. S. CHAND – conceptual physics XI na XI

2. NELKON AND PARKER

3. RAMSDEN PHYSICS

4. UNIVERSITY PHYSICS (UP)

5. PHYSICS FOR SECONDARY SCHOOL FORM FIVE & SIX (TIE 2016)

6. TOM DUNCAN, PRINCIPLE OF PHYSICS.

D. VITABU VYA GEOGRAPHY

1. Pritchard J.M. (1979), Afrika a study Geography for advanced students. London longman.

2. Msabila D.T (2003) Success in Geography Climatology and Soil science Dar es salaam-afroplus industries L.T.D

3. Prichard J.M. (1990) Practical Geography for Africa. Longman.

4. Kamili, 2, Physical Geography for Africa. Dar es salaam Afroplus industries.

5. Msabila D.T. Physical Geography. Dar es salaam, Nyambari Nyangwine Publishers.

6. Msabila D.T. (2006) Human and Economic Geography (Advaced level paper 2.) Nyambari Nyangwine publishers.

E. VITABU VYA BASIC APPLIED MATHEMATICS (BAM)

1. Basic Applied Mathematics for secondary school

2. Basic Applied Mathematics Review

3. Basic Applied Mathematics (TIE)

F. VITABU VYA ECONOMICS

1. Ambilikile C.M (2010) Economics for Advanced Level (Part I&II)

2. Gupta S.L and Chaturved D.D (2003) Managerial Economics, Texts and Cases

3. Othieno Okoth (2005), Contemporary Economics

4. Mudida R (2003) Modern Economics 1st Ed. Nairobi Kenya

G. VITABU VYA GENERAL STUDIES (GS)

1. Richard R.F Mbalase, General Studies For Advanced Level Certificate

2. Mgaywa, B.M – General Studies for Advanced Level, 3rd Ed

3. Joannes, B & S.M Deogratias "Understanding Advanced Level General Studies; Advanced Secondary School Education

H. VITABU VYA ADVANCED MATHEMATICS

1. S. CHAND, ADVANCED MATHEMATICS I & II

2. PURE MATHEMATICS I & II

3. TRANTA ADVANCED MATHEMATICS

VI. VYOMBO VYA CHAKULA

a) Sahani na kijiko

b) Kikombe na Bakuli

VII. MWANAFUNZI LAZIMA AJE NA RESULTS SLIP YA MATOKEO YAKE YA KIDATO CHA NNE NA CHETI CHA KUZALIWA ORIGINAL SIO KIVULI ASIPOKUJA NAYO HATAPOKELEWA

C. FOMU ZIFUATAZO ZIMEAMBATANISHWA NA NIMUHIMU KUZIKAMILISHA

1. Historia ya wazazi na mtoto

2. Kukubali kujiunga na shule

3. Fomu ya kupima Afya (medical examination)

TAFADHALI NI MUHIMU SANA KUPIMA AFYA YAKO NA KUJA NA VYETI ILI KUONDOA USUMBUFU

MWISHO

Shule hii inathamini Umoja, amani na juhudi katika masomo na kazi za nje pamoja na michezo. Nidhamu safi ni msingi wa mafanikio ya kila binadamu, hivyo kila atakaye kubali kujiunga na shule hii atatakiwa kuzingatia maelekezo hayo. Sheria za shule zimeambatanishwa, zisome kwa makini na uwe tayari kuzifuata.

……

BEATRICE A. MWALUGAJA

MKUU WA SHULE

KIAMBATA 'A'

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO

SHULE YA SEKONDARI NSIMBO

Kumbukumbu Namba:

HISTORIA YA WAZAZI NA MTOTO ALIYE CHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE HII A. WAZAZI/WALEZI

1. Jina la Baba……Hai/Si hai

2. Jina la Mama……Hai/ Si hai

3. Kama Baba si hai jina la Mlezi……

4. Kazi/shughuli ya Mzazi/Mlezi……

5. Anwani ya Mzazi/Mlezi……

6. Uraia wa Wazazi -Baba mtanzania/Si mtanzania -Mama mtanzania/Si mtanzania

7. Wakati wa likizo Mtoto/Mwanafunzi unatakiwa uende wapi? ……

8. Jina la mtu aendako…… Uhusiano na Mtoto/Mwanafunzi

SAHIHI YA BABA/MAMA/MLEZI TAREHE

…… ……

SAHIHI YA MWANAFUNZI TAREHE

…… ……

PICHA YA MZAZI/MLEZI PICHA YA MWANAFUNZI

KIAMBATA 'B'

FOR MEDICAL EXAMINATION

To be completed by medical officer in respect to all forms of entrants Student's full name……Age……..Years…… ……..Sex…….. . Blood count (red and white) …….. Stool examination…….. Urine analysis……. Syphilis and other venereal disease test…… …… T.B test…….. Eye Test…….. Ears ……..…….. …….. Abdomen…… …… …… Urine for plant test……. Test for pregnancy…….

ADDITIONAL INFORMATION

Defects, impotents (e.g. arms, legs etc) infections, chronic or family diseases etc …… …… …… ……. I certify that the named above is fit to pursue further studies in agricultural/domestic education Station…… signature…….. Date…… designation…….

KIAMBATA 'C'

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO

SHULE YA SEKONDARI NSIMBO

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

Mimi…….nimesoma kwa makini maagizo yote ninatambua kuwa kuchaguliwa kwangu kuingia shule ya sekondari ni bahati na zawadi kubwa kwa kuwa wengi wamekosa nafasi si kwa kuwa wameshindwa ila kwa sababu ni chache.

Hivyo nakubali kujiunga na shule yaSekondari Nsimbo ya Wasichana. Nitatii na kufuata sheria na taratibu zote za shule. Nitajitahidi kufanya kazi/kusoma kwa juhudi na maarifa na nitajitahidi kushirikiana na wenzangu kweli daima.

Nitalinda hadhi/heshima ya shule ya Sekondari Nsimbo na nitashirikiana na wenzangu kujenga misingi na historia nzuri ya shule.

Tarehe…… Sahihi ya mwanafunzi…….

Mimi…….. Mzazi/Mlezi……..…….. Nimeshuhudia mtoto wangu…… akikubali kwa hiari kujiunga na shule hiyo ninaamini mtajitahidi kumfunza na kumlea vizuri. Mimi pia naahidi kushirikiana nanyi kikamilifu katika kumlea binti yangu naamini tutakuwa tunawasiliana.

Tarehe…… .. Sahihi ya Mzazi/ Mlezi……..……..

KIAMBATA 'D'

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO

SHULE YA SEKONDARI NSIMBO

SHERIA ZA SHULE

MIPAKA YA SHULE

Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea vijiji jirani wala kwenda mjini bila kupata kibali cha mkuu wa shule.

Mwanafunzi haruhusiwi kwenda kwenye nyumba za wafanya kazi wa shule bila idhini ya mkuu wa shule.

Mwanafunzi haruhusiwi kuonekana maeneo ya idara za masomo baada ya saa 12 jioni.

MAVAZI RASMI YA SHULE DARASANI

Sketi ya Dark blue ndefu shati jeupe la mikono mirefu na hijabu nyeupe kwa wanafunzi wa kiislamu. Viatu vyeusi vya kamba visivyo na visigino virefu na visiwe vya kugonga Soksi nyeupe fupi.

KAZINI

Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sketi ya rangi ya damu ya mzee ndefu na t-shirt, au hijabu nyeupe kwa waislam.

MICHEZONI

Mwanafunzi awapo michezoni avae traki suti ya rangi ya dark-blue na T- shirt ya njano.

NJE YA SHULE

Mwanafunzi akiwa nje ya shule avae sketi ya rangi ya damu ya mzee na T- shirt ya rangi ya kijivu yenye nembo ya shule na viatu vyeusi, kwa waisilamu wavae sketi ndefu na hijabu nyeupe.

SAFARI

Mwanafunzi anapokuwa safarini avae sketi ndefu pamoja na T-Shirt ya shule yenye nembo.

UTARATIBU KATIKA BWALO LA CHAKULA

• Ni muhimu kufuata utaratibu na muda uliopangwa wa kula kufuatana na ratiba ya shule.

• Kila mwanafunzi awe na sahani, bakuli, kijiko na kikombe. Vyombo hivi vitunzwe bwenini.

• Wanafunzi wakae mezani wakati wa chakula

• Wanafunzi hawaruhusiwi kupiga kelele wakati wa chakula

• Mwanafunzi haruhusiwi kuingia na ndala au kiatu cha wazi ndani ya bwalo la chakula.

JIKONI

Viranja wa chakula na afya ndio wanao ruhusiwa kuingia jikoni wakati wa chakula.

MABWENINI

• Wanafunzi hawaruhusiwi kulala wawili kitanda kimoja

• Kila mwanafunzi ni lazima alale katika bweni na chumba alicho pangiwa

• Wanafunzi hawaruhusiwi kuoga, kutembea mabwenini au nje ya bweni baada ya saa 5:00 usiku

• Ni marufuku kupiga na kusikiliza muziki bwenini

• Upotevu/uharibifu wowote wa mali ya umma bwenini utalipwa na wakazi husika wa bweni.

• Mwanafunzi haruhusiwi kuwepo bwenini wakati wa masomo au wakati ratiba ya shule ikiendelea.

• Mwanafunzi haruhusiwi kuingia na chakula au kula chakula bwenini

• Kila mwanafunzi azingatie usafi wa bweni siku zote na siku maalumu za usafi

DARASANI

• Wanafunzi wawe madarasani mnamo saa moja na dakika ishirini na tano asubuhi.

• Mwalimu anapo ingia darasani wanafunzi wasimame na kumuamkia mwalimu.

• Wanafunzi wasipige kelele wawapo darasani

• Wanafunzi wasitoke nje ya darasa wakati wa masomo bila ruhusa maalumu

• Ni wajibu wa kila mwanafunzi kujibu na kuuliza maswali na kukamilisha kazi alizo achiwa na mwalimu wa somo.

• Usafi wa darasani ni wajibu wa kila mwanafunzi

NJE YA DARASA

• Wanafunzi wasimame na kumsalimia mwalimu au mtu aliye wazidi umri anapo pita.

• Wanafunzi wawaheshimu wafanyakazi wengine waliopo shuleni kama inavyostahili

• Wanafunzi watumie lugha ya heshima kwa walimu, watu wengine na hata wao kwa wao.

• Wanafunzi wawe watii, wasiwe wagonvi, wasengenyaji, wavivu, walevi na wazururaji

• Wanafunzi wawe na moyo wa kushirikiana na kusaidiana wakati wa shida na raha

• Wanafunzi waheshimu bendera ya Taifa na alama zingine za taifa pamoja na ukumbi wa mikutano

• Mwanafunzi anatakiwa kuongea kiingereza wakati wote awapo shuleni.

MATIBABU

• Wagonjwa wote watatibiwa katika hospitali ya serikali ya Wilaya pamoja na dispensary ya shule tu.

NB: Bima ya Afya ya Taifa ni muhimu kwa ajili ya matibabu au mzazi atalazimika kulipa gharama za matibabu ya motto wake.

MAKTABA

• Wanafunzi hawaruhusiwi kuingia maktaba wakiwa wamebeba mikoba ya vitabu/madaftari

• Wanafunzi waingie maktaba wakiwa wamevaa vazi rasmi la shule

• Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya maktaba na kitabu au gazeti bila ruksa ya mkutubi au mwalimu mhusika wa maktaba

• Mwanafunzi ataingia maktaba katika muda maalumu uliopangwa

WAGENI

• Wageni wa aina yeyote ile hawaruhusiwi kuingia au kupita shuleni bila shida maalumu na idhini ya mlinzi wa zamu

• Wageni wa aina yeyote ile hawaruhusiwi kuonana na mwanafunzi isipokuwa kwa wale wenye shida za kiofisi tu.

• Maagizo yote ya wageni kwa mwanafunzi au wanafunzi yatapokelewa na mwalimu wa zamu (vyakula na vivywaji pombe na dawa za kienyeji havitapokelewa).

HUDUMA ZA OFISI

• Ofisi ya shule itapokea taarifa za dharura za wanafunzi kama vile msiba au tatizo kubwa la kifamilia pamoja na maagizo yote ya wazazi/walezi kwa mwanafunzi

• Mwanafunzi haruhusiwi kupiga au kupokea simu bila idhini ya mkuu wa shule

• Mwanafunzi haruhusiwi kuingia ofisi yoyote shuleni isipokuwa ni lazima wagonge/wapige hodi kabla ya kuingia

• Barua za wanafunzi zitapokelewa na mwalimu wa zamu ambaye atazikabidhi kwa kiranja wa zamu ili azigawe kwa wahusika

MAMBO YASIYO RUHUSIWA KUFANYWA

i Uwasherati na uzururaji

ii Wizi

iii Kuchezea au kuharibu bendera ya Taifa

iv Kugoma

v Kumpiga au kumtukana mwalimu/mfanya kazi

vi Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

vii Kutoroka shule au kuachana na wenzake wakati anapotoka nje ya shule kwa shughuli za kishule

viii Kunywa au kulewa pombe/kuvuta sigara

ix Kupigana

x Kupiga kelele ovyo au kuita kwa sauti kubwa

xi Ubaguzi wa aina yoyote

xii Kuzungumza lugha nyingine yoyote isipokuwa kiingereza, Kiswahili kinaruhusiwa katika mazingira maalumu tu

xiii Kuvaa mavazi yasiyo sare ya shule

xiv Kutofika au kuchelewa sehemu ya parade

xv Ni marufuku kwa mwanafunzi kuja na simu, kamera, pamoja na redio shuleni.

ADHABU

ADHABU ZITATOLEWA KULINGANA NA UZITO NA MAKOSA YALIYOFANYIKA, ISIPOKUWA MWANAFUNZI AKIFANYA MAKOSA YAFUATAYO ATAFUKUZWA SHULE MARA MOJA;

I. UASHERATI NA USHOGA
II. UZURURAJI
III. WIZI
IV. ULEVI
V. UTORO (KUTOONEKENA ENEO LA ROLL CALL)
VI. KULALA NJE YA SHULE
VII. UVUTAJI WA BANGI/SIGARA
VIII. MAKOSA YA JINAI
IX. KUPIGANA AU KUPIGA
X. KUHARIBU KWA MAKUSUDI MALI YA UMMA
XI. KUDHARAU BENDERA YA TAIFA
XII. KUOLEWA
XIII. KUPATA MIMBA
XIV. KUTOA MIMBA
XV. UBAKAJI.
XVI. KUGOMA, KUCHOCHEA NA KUONGOZA AU KUVURUGA AMANI NA USALAMA WA SHULE
XVII. KUKATAA ADHABU KWA MAKUSUDI
XVIII. KUMILIKI AU KUKUTWA NA SIMU YA MKONONI

Elewa kuwa si rahisi kutunga sheria za kila kosa linalo weza kufanywa na mwanafunzi. Sheria ni mwongozo wa kumuelewesha mwanafunzi mambo ambayo haruhusiwi kufanya. Kitu muhimu ni kwamba kila mwanafunzi atumie akili yake na busara kuweza kujua namna gani ya kuishi na walimu, wafanyakazi wasio walimu pamoja na wanafunzi wenzake ili kutumia nafasi yake kupitia elimu na kuishi kwa raha na amani katika jitihada za kujiendeleza mwenyewe, shule pamoja na taifa zima kwa ujumla.

Kumbuka kuwa umepata bahati kubwa kuwa kati ya wanafunzi walio chaguliwa kujiunga na shule hii kwa hiyo toa mchango wako katika kujenga msingi imara, sifa na mwenendo mzuri na maendeleo safi kwa shule yako ya Sekondari Nsimbo.

ELIMU NI MWANGA WA MAISHA

.....

BEATRICE A. MWALUGAJA

MKUU WA SHULE